


Na: 28. Msimu wa Kilimo 2018/19 Tathmini ya Kipindi cha Juni 21-30, 2019 na Matazamio kwa Kipindi cha July 1-10, 2019

Muhtasari

- Hali ya ukavu itaathiri mazao yaliyopandwa kwa kuchelewa na upatikanaji wa maji kwa mifugo katika kipindi cha siku kumi zijazo .
- Hali ya ukavu inayotarajiwa itasaidia uvunaji, ukaushaji na utunzaji wa mazao.

MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA JUNI 21-30, 2019

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo sehemu ya kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliendelea kuimarika wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia (Azores na Siberia) iliendelea kudhoofika. Ukanda wa mvua uliendelea kuwa kaskazini zaidi mwa Ziwa Victoria. Pamoja na kuimarika kwa migandamizo mikubwa ya hewa upande wa kusini bado kulikuwa na maeneo machache yenye migandamizo midogo ya hewa katika eneo la karibu na Madagascar iliyopelekea vipindi vya upepo mkali katika maeneo mengi ya nchi. Joto la bahari katika maeneo ya kusini magharibi mwa bahari ya Hindi lilikuwa la wastani na kusababisha kutokuwepo kwa vipindi vya vimbunga. Upepo ulivuma kwa wastani kutoka kusini hadi kusini mashariki katika maeneo mengi ya nchi. Eneo la kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) lilikuwa na joto la bahari la wastani hadi juu kidogo ya wastani. Hali hii ilisababisha kupungua kwa mifumo ya kusababisha mvua katika maeneo ya magharibi mwa nchi.



Kielelezo: Kiasi cha mvua katika kipindi cha Juni 21- 30, 2019

MWENENDO WA MVUA KATIKA KIPINDI CHA JUNI 21-30, 2019

Kwa kipindi hicho maeneo mengi ya nchi yalikua makavu isipokua kwa baadhi ya maeneo machache ya nyanda za juu kaskazini magharibi hususan mkoa wa Mara ambapo yamepata mvua za nje ya msimu. Kiasi cha mvua kilichopimwa ni kati ya 26 mm na 50 mm kama inavyojionesha kenye kielelezo.

TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA JUNI 21-30, 2019

Katika kipindi cha dekadili iliyopita, maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua, hususan katika mikoa ya Ruvuma, Mtwara, Dodoma na Rukwa wakulima walikuwa wanamalizia shughuli za uvunaji wa mahindi. Zao la ngano lilikuwa katika hatua ya kukomaa kwa mikoa ya Iringa, Njombe na Mbeya. Maharage yameripotiwa kuwa katika hali nzuri katika hatua ya kukomaa kwa mikoa ya Mbeya. Katika maeneo mengi yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka zao la mahindi lilikuwa katika hatua ya kukomaa na shughuli za uvunaji wa mahindi ziliendelea katika mikoa ya Simiyu, Moshi, Pwani na Mara. Mahindi yaliyopandwa kwa kuchelewa msimu wa mvua kwa mkoa wa Tanga yameathiriwa na hali ya ukavu. Maeneo ya mikoa ya Mbeya, Ruvuma, Tabora, Kigoma, Morogoro, Pwani, Simiyu na Shinyanga wakulima walikuwa wanamalizia uvunaji wa mpunga. Hali ya ukavu iliyojitokeza

imesaidia katika shughuli za uvunaji, ukaushaji na utunzaji wa mazao kwa maeneo yote yanayopata msimu mmoja na misimu miwili ya mvua kwa mwaka. Upatikanaji wa malisho na maji kwa ajili ya mifugo ulieendelea kupungua kutokana na kuendelea kwa kipindi cha hali ya ukavu.

HALI YA MAJI ILIVYOKUWA KATIKA KIPINDI CHA JUNI 21-30, 2019

Kina cha maji katika mabwawa, mabonde na mtiririko wa maji katika mito iliendelea kupungua kutokana na kuendelea kuwepo kwa hali ya ukavu na upepo mkali. Katika maeneo mengi nchini.

MIFUMO YA HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA JULAI 1-10, 2019

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini (St. Helena na Mascarene) inatarajiwa kuendelea kuimarika wakati ile migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) inatarajiwa kuendelea kudhoofika. Pia ukanda wa mvua unatarajiwa kuendelea kuwa kaskazini mwa Ziwa Victoria hali itakayopelekea upepo kuvuma kutoka kusini hadi kusini mashariki katika maeneo mengi ya nchi. Hata hivyo joto la bahari la wastani hadi chini ya wastani linatarajiwa katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi, hivyo itapunguza uwezekano wa kutokea vimbunga. Upepo unatarajiwa kuvuma kutoka kusini hadi kusini mashariki na hali hiyo itasababisha baridi katika maeneo mengi ya nchi. Eneo la Kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) kunatarajiwa kuwa na joto la bahari la wastani hadi juu kidogo ya wastani. Hali hii itapelekea kupunguza kwa upepo uvumao kutoka magharibi hivyo kupunguza nguvu ya mifumo isababishayo mvua katika maeneo ya magharibi mwa nchi.

HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA JULAI 1-10, 2019

Maeneo ya Kanda Kanda ya ziwa Victoria (mikoa ya Kagera,

Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara) yanatarajiwa kuwa na mvua zinazoambatana na ngurumo katika maeneo machache.

Nyanda za juu kaskazini mashariki (mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro), magharibi mwa nchi (mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora), pwani ya kusini (mikoa ya Mtwara na Lindi) yanatarajiwa kuwa makavu kwa ujumla.

Pwani ya kaskazini (mikoa ya Tanga, maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja navisiwa vya Unguja na Pemba yanatarajiwa kupata mvua nyepesi katika maeneo machache.

Kanda ya kati (mikoa ya Dodoma na Singida), nyanda za juu kusini magharibi (mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa), kanda ya kusini (mikoa wa Ruvuma na maeneo ya kusini mwa Morogoro) yanatarajiwa kuwa na hali ya mawingu kiasi.

MATARAJIO NA USHAURI KWA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA JULAI 1-10, 2019

Hali ya ukavu inayotarajiwa katika maeneo ya nyanda za juu kaskazini mashariki (mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro), magharibi mwa nchi (mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora), Pwani ya kusini (mikoa ya Mtwara na Lindi) itasaidia kukomaa kwa mazao pamoja na shughuli za uvunaji na uhifadhi wa mazao. Hali ya ukavu inatarajiwa kuathiri mazao yaliyopandwa kwa kuchelewa. Hali ya maji pamoja na malisho vinatarajiwa kuendelea kupungua. Hata hivyo, wakulima, wavuvi na wafugaji wanashauriwa kuwasiliana na maofisa ugani kwa ajili ya kupata ushauri zaidi.

HALI YA MAJI INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA JULAI 1-10, 2019.

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vinatarajiwa kuendelea kupungua katika maeneo mengi nchini kutokana kuendelea kwa hali ya ukavu na upepo. Hivyo, wananchi wanashauriwa kutumia maji hayo kwa uangalifu hususan maeneo ambayo huwa yanakabiliwa na upungufu wa maji.

Jarida limetayarishwa na:

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania
Ghorofa ya 3-Ubungo Plaza – Barabara ya Morogoro, Dar es Salaam-Jamhuri ya Muungano wa Tanzania